THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2:30 **Jumatano , 08 Novemba 2017 mchana**

CS17PREP

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali **kumi na mbili (12).**
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

1 701015 100011

CS17PREP

Scanned by CamScanner

BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIM

SEHEMU A: QUR-AN

1. Onesha tofauti nne kati ya Sura zilizoteremshwa Makka na zilizoteremshwa Madina.

2. Andika tafsiri ya Surat Quraysh kisha eleza mafunzo manne yanayopatikana.

3. *"Nawe hukua unatumai ya kwamba utaletewa kitabu, lakini ni rehema ya mola wako" (28:86).* Kwa kuzingatia aya hii tumia hoja nane kuthibitisha kwamba Qur'an **si** neno la Muhammad (s.a.w).

SEHEMU B: TAWHIDI

CS17PREP

4. *"Na katika Ardhi zipo (alama namna kwa namna) za kuonesha kuwepo kwa Allah (s.w) kwa wenye yakini Na katika nafsi zenu (pia zimo alama) Je hamuoni?" (51; 20-21).* Tumia hoja nane kuthibitisha dalili za kuwepo kwa Allah (s.w) kutokana na nafsi ya mwanadamu.

5. *"Basi alipofika, aliitwa Ee Mussa hakika mimi ndiye Mola wako. Basi vua viatu vyako, hakika wewe uko katika bonde takatifu la Tuwa" (20: 11-12).* Kwa kuzingatia aya hii chambua njia tano za mawasiliano kati ya Allah (s.w) na Mitume wake.

6. *"Je (watu) wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinajisalimisha kwake kipende kisipende na kwake watarejeshwa" (3:83).* Kwa kutumia aya hii;
   (a) onesha tofauti tano kati ya mtazamo wa Kiislamu na usiokuwa wa Kiislamu kuhusu nadharia ya dini.
   (b) thibitisha kwa kutumia hoja tatu ni kwa namna gani vipawa alivyotunukiwa mwanadamu humfanya awe na dini?

SEHEMU C: FIQH

7. Chambua miradi mitano ya biashara au uzalishaji inavyoweza kutumiwa na benki ya Kiislamu katika kujiendesha na kunufaisha jamii.

8. Kwa kuzingatia sheria ya familia ya Kiislamu, fafanua mambo sita ya msingi ambayo ni wajibu wa wazazi kwa watoto wao.

9. Jadili masharti sita yanayopaswa kuzingatiwa na muoaji katika ndoa ya Kiislamu.

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. *"Tulimpeleka Nuhu kwa watu wake, naye akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu nyinyi hamna Mungu ila yeye ....." (7:59).* Kwa kuzingatia aya hii fafanua mbinu sita alizotumia Nabii Nuhu kufikisha ujumbe kwa watu wake.

11. Eleza mafunzo sita yatokanayo na mambo aliyoyafanya Mtume (s.a.w) katika kuanzisha dola ya Kiislamu.

12. Kwa kuzingatia utaratibu wa kuchagua Khalifa wa Kiislamu;
    (a) eleza sababu nne zilizosababisha Abubakar kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Dola ya Kiislamu.
    (b) fafanua tofauti mbili za kimawazo zilizojitokeza kuhusiana na uchaguzi wa Abubakar kuwa Khalifa wa kwanza katika dola ya Kiislamu.

CS17PREP

Scanned by CamScanner